JUA

GAZETI LA MAENDELEO

Kiongozi: Mutiri-wa-Bashara - Mwaka wa 21 - Toleo la 440

Eti woga wawatetemesha viongozi nchini

Nchini Zaïre woga watuma watu wengi kuota mabawa, kutwika miguu shingoni na kufyatuka kama ndege wasijue mahali wakwendako na mizigo wabeba. Jambo hilo laonekana na Wana-Zaïre ambao siku kwa siku watishwa na mambo yapitika nchini toka hali kisiasa yaikumba nchi tangu miezi kazaa. Kwa kuwa hatua, masemi na vitendo vyafanywa na wakuu viongozi nchini vyaenda kinyume cha maagizo na mahakikisho walioyafanya. Na sio na watu wengine bali na wale wale viongozi waliohaidia wakaaji na raïa wote kama watawaletea heri wahitaji.

Lakini kuambatana na mizozo ya kisiasa ambayo yaendeshwa siku kwa siku, yaonekana kweli kama viongozi wamoja hasa hao wa jamhuri ya Pili kunacho kitu waogopa. Kwani kwa kuwasikia wakisema watambua kuwa ndani mwao watetemeshwa na woga fulani. Waogopa nani na nini ?

Yaonekana kuwa viongozi wa Jamhuri ya Pili waogopa waziri mkuu wa serkali ya mpito na kundi lake. Bwana Tshisekedi wa Mulumba na jeshi lake la mawaziri waonya ujuzi katika kazi waendesha na hata rushwa yatezamiwa kukataliwa huko.

Akiwa mwakilishi wa upinzani wote, huyu ategemea sana uwezo wa Mkutano mkuu wakitaifa ambao kama kamteua. Na ijapokuwa tangu tarehe 24 Aprili 1990 ukweli wajionya na watuelimisha wote, viongozi hao katishwa na Mkutano mkuu huo ambao hatua zake kachukua zapaswa kutimizwa na Serkali ya mpito na kuchunguzwa kwa utimizo na Baraza kuu la Ushauri la Jamhuri (HCR). Na woga wawashika viongozi hao ni kuona katika hatua kachukuliwa, katiba iliyoko yapaswa kutengwa na kugombolewa na hati ya kanuni zingine za sheria kwa uongozi bora muda wote wa mpito hadi uchaguzi kafanywe hapo makesho baada ya miaka miwili. Pia kurushwa kwa Bunge la Taifa na kuachia hivi nafasi Baraza kuu la Ushauri la Jamhuri. Bila kusahau kuwa Mkutano mkuu wa kitaifa ni kiungo muhimu kuliko vingine vyote vilivyoko : uraïs wa jamhuri, serkali na kazalika.

Kwanza vyeo vyao

Tukichungua kwa karibu hali ya kisasa iliyoko nchini, uwasiwasi mkubwa wawashika raïa kwa kuwa katika kundi la washauri lazunguuka Raïs Mobutu, Mareshali wa Zaïre, kwapatikana pia washauri wazuri lakini wengi mabao wajionya wabaya hawapendi kamwe mabadiliko yafanywe nchini. Kwa kuwa kisha miezi minne tu kusimikwa kwake kiserkali Baraza la mwaiziri laongozwa na bwana Tshisekedi yaonekana mambo kutoongoka nchini kwa kuwa hakunako masikilizano kati ya Raïs wa Jamhuri na Waziri mkuu. Kwani kwa mshangao mkubwa, mnamo tarehe 10 Desemba 1992, Raïs Mobutu kachukua hatua ya kuwakabizi wakatibu wakuu wa kazi za serkali madaraka ya kuongoza kazi za mawaziri baada ya kulitenga baraza laongozwa na bwana Tshisekedi na kwa hatua yake ya tarehe 4 Desemba baada ya kuvunja serkali hiyo kamteuwa mara ingine kama vile waziri mkuu kwa mpya na kuomba aunde serkali ingine mpya Hiyo haikusilika na watu wote.

Kutokana na vitendo hivyo, yaonekana wazi kuwa hali ya kisiasa nchini siyo bora na kutia watu katika hali yakutowaaminia wanasiasa hasa viongozi walioko. Kwani mazozo ulio kati ya Raïs Mobutu na bwana Tshisekedi ni tunda tu la tamaa ya wanasiasa wamoja ambao wakazania kubaki na madaraka ya uongozi mikononi mwao bali pia wajulikana kwa tamaa yao ya kupinga ao kuikwamisha siasa ya kuimarisha na kuiinua maisha ya raïa wakitafuta pia kuilaza matumaini ya taifa nzima kwa manufaa yao pekee. Kwa ngambo yake, Raïs wa Jamhuri aonekana kwa vile mwenyi hakubaliane na matokeo ya Mkutano mkuu wa Kitaifa, hamjui askofu Monsengwo na wengineo viongozi wa makanisa kama vile wapatanishi, kait ya vikundi wapigana, hakubali kama Baraza kuu la Ushauri la Jamhuri ni kiungo kuliko vyote na ambacho kagomboa Bunge la Taifa na kuchukua madaraka yake. Ni hapo magonvi yatezamiwa kutukia kati ya baraza hilo kuu na Raïs wa Jamhuri. Kwani kutokana na uchaguzi kafanyika hapo majuzi, wanamemba wa baraza hilo kamchagua bwana Ileo Songo wa chama PDSC kama vile makamu wa kwanza wa mwenye kiti wa baraza hilo, askofu Monsengwo na bwana Lutandila kama vile makamu wa pili. Iliyo hofu ni kuona kama bwana Ileo kama kiti cha uraïs chabaki wazi aweza kuchukua madaraka ya uraïs!

Mnamo tarehe 23 Desemba 1992, Jemadari Mahele kiongozi wa makao makuu ya askari-jeshi kaitisha mkutano wa wasimulizi rasmi kati ya wanasiasa, wawakilishi na wajumbe wa viungo muhimu madarajani kote nchini, mabingwa wa siasa kapinga mkutano huo labda kutokana kwa kununa na kutoka Mkutanoni huo mkuu wa kitaifa kwa maofisi ambao kapendelea kutoendelea na kazi zao kwenyi mkutano wa matumaini. Hawa wakionya kwa kitendo chao kupendelea kubaki upande wa Raïs wa Jamhuri. Na toka kitendo hicho hangeweza kamwe kuitisha mkutano wake. Na kulingana na hatua kachukuliwa Mkutanoni mkuu vikosi vya askari-jeshi vyapaswa kuwa chini ya madaraka ya waziri wa Ulinzi na Usalama wa nchi. Kumbe Jemadari Mahele bila ruhusa ya waziri wake hangewakusanya watu kwa jina la uongozi wa vikosi.

Waziri mkuu akiendelea kuwakusanya kama kawaida mawaziri wake, hivyo yaonya kuwa hawa hawakuachishwa hakika kazi zao na hatua kachukuliwa na Raïs wa Jamhuri. Kwani wamoja makatibu wakuu wa kazi za serkali kunako mawaziri kakataa kuchukua nafasi ya mawaziri na madaraka yao na wengine huendesha kazi kawaida. Ni toka hapo kaonekana kusimikwa kwa serkali mbili nchini moja. Pia askari-jeshi washindwa kulinda na kukinga watu na mali zao bali wajiruhusu kuunda vikundi vya ujeuri, vya ukaidi na vya uwizi kwa kuwazulumu wakaaji. Kwani vitendo mijini mingi haiwaeshimishe hata kidogo.

Iwe mjini Kinshasa mnamo tarehe 18 Desemba 1992 : Watu kaandamana kwa kupinga udikteta wa Raïs Mobutu. Watu 15 kauwawa na wengine kaumizwa vikali, wasemavyo, ingawa kajulishwa kiserkali eti ni watu wanane tu kafariki dunia.

Mjini Kisangani, mnamo tarehe 20 Desemba, askari-jeshi, kutokana na kuchelewa kulipwa mishahara ambayo kalipwa kwa noti ya zaïre milioni 5 kasakanya mji, kauvuruga na kuiba vitu kazaa baada ya kushika mateka komanda wa vikosi na liwali wa jimbo. Na mjini Goma, katika usiku wa tarehe 22 hadi 23 Desemba, baada ya kufikishwa huko noti hiyo ya zaïre milioni 5 mnamo tarehe 14 Desemba, maandamano kafanywa kwa kupinga siasa iliyoko : ofisi ya vyama MPR na DCF kaoigwa msako, "restaurant" Nyira ya Bwanandeke kaona cha mtema kuni. Biashara vingi kaibwa madukani kama vile vifaa vingi nyumbani mwa watu vikachukuliwa, kuchomwa na watu kusagwa makande na kutupwa jela. Magari ya wenyi mali kasaidia kuvichukua. Vitendo hivyo kafanya pia mjini Kiwanja katika mtaa wa Rutshuru pia mjini Kolwezi jimbonimwa Shaba.

Bukavu pole

Jimboni mwa Kivu ya Kusini, mji wa Bukavu ambao katezamiwa kutilishwa pia, waandamanaji, wakiwemo hasa wanafunzi, kapinga udikteti wa Raïs Mobutu na noti ya zaïre milioni 5 katika maandamano ya usalama na upole vikinyooshwa juu vibao na vitambaas vyenyi maandiko ya upinzani na bila kusukumwa wala kutiwa wofu na askari-jeshi wala wote wanaohusika na kulinda amani. Hiyo kutokana na misaada ya vyakula na vinginevyo vifaa katolewa na wafanyabiashara wa mji jimboni mwa Luberizi. Na mjini Uvira waandamanaji ambao huko wapinga pia siasa ya MPR na udikteta wa prezidenti wake kasakanya nyumba za viongozi wa chama hicho, wanainchi Noki na Lugi badala ya mto Kaiimabengo toka mafuriko ya maji ya mvua kubomoa vyote kakuta njiani na kutia hasara nyingi mjini.

UHARIRI

Uwe wa heri na fanaka

Ouf ! Twafika mwaka mpya wa 1993. Mambo mengi yamepita na mwaka wa 1992 kwa namna wa mwendo wa kunguru. Tukitupa jicho nyuma tutajionea wenyewe namna gani mwaka 1992 wateremusha na usito wa magumu, raha, mipando na miporomoko ya maisha. Sisi sote, hasa Wana-Zaïre, kamshukuru Mungu Mweny'Ezi kwa shangwe na vigelegele kutokana na mambo kajionea.

Kwa kweli, ingawa wenyi pato kubwa kasherekea sikukuu hiyo ya bonaña kwa vinywaji na vyakula, wengine kununa na kusaga meno, mawazo kawayeyusha ubongo. Hiyo ilikuwa mapenzi ya Mungu mwenyewe. Mambo mengi yamepita ulimwenguni katika mwaka huo wa 1992 na Gazeti JUA katimiza mapaswa yake ya kuwajulisha wasomaji wake wapendwa na watukufu.

Mwakani humo, kunako pande zote nne za dunia, vita, uwizi, mauwaji, maendeleo, raha, fanaka na mambo mengine mengi kapitika, mazuri kama vile mabaya. Watu wengine watabaki na sura mbaya ya mwaka huo hata kila watakapokumbuka sherti watatekwa jasho la damu na baridi. Na kwa wengine labda mwaka huo ulijaa mafanikio. Oh! Dunia.

Nchini Zaïre, baada ya raïa kuvutia hewa ya kidemokrasia, mwaka 1992 ulionya na tatizo mengi kwa raïa hao. Ni kama vile ya kisiasa : Mkutano mkuu wa kitaifa ambao kadumu muda wa miezi 17 na toka huo mkutano kasimikwa Baraza kuu la ushauri wa Jamhuri, serkali kasaa za mapitilio kwa jamhuri ya tatu kasimikwa kwa kungojea uchaguzi hapo mwaka 1994. Lakini mambo katezamiwa kutoongoka ginsi kahitajika na raïa. Pia maandamano kazaa wa kazaa kafanywa kwa kupinga ujeuri na udikteta wa viongozi. Raïa kajionea cha mtema kuni, waandamaji wamoja kauwawa, makao, maduka, viwanda na vifaa kazaa kabomolewa, kaunguzwa ao kapeperushwa. Sokoni kama vile madukani wanunuzi hushikwa na bumbwazi wa bei za vitu kapanda kama vile mshale. Samani kashuka siku kwa siku. Kitisho hichoi kakiepushe jamaa nyingi na maisha kawa magumu kweli. Mwaka huu mpya utaturuhusu kusahau balaa hile ?

Jimboni mwa Kivu ya Kusini, ingawa serkali kahusika na uhusiano bora wahitajika baina ya majimbo yanayopakana na pia nchi jirani, hali ya lmaisha kiuchumi na kijamii yazorota. Unjenzi ovyo ovyo wafanyika mahali mengi, mimemonyoko ya arzi na uharibifu wa mabarabara kutokana na maji ya mvua kawatisha na hata kuwatia jamaa nyingi katika vilio na mengineo magumu kazaa kaangamiza raïa. Pia nchini ingawa mabadiliko makubwa yangojewa kweli mwakani huu, viongozi wa zamani toka jamhuri ya pili wangali bado wanakwamisha juhudi safanywa kuyafikilia.

Barani Afrika, makaburu wa Afrika ya Kusini kaendelea kujitatanua ili kubadili siasa yao ya kibeberu na kukubali watu weusi washiriki kwenye uongozi wa inchi yao. Vita vikali vya watetemesha raïa wa Liberia, Somalia na zinginezo nchi. Uvumi wa Perestroïka wakumba na kutisha madikteta wengi, na wale wanao baki wanatetemeka wakihesabu siku chache zinazowabakilia.

Katika Bara la Azia, Irak kaamua kuendelea kuvamia Koweït na kusisitiza kuigeuza nchi hiyo ndogo kuwa jimbo lake. Nchi za magaribi kachukua wajibu huo kuamsha kitisho cha vita zidi ulimwengu mzima. Shujaa Saddam Hussein kaendelea kudai kwamba haogopi Amerika na wote wataka kumtenga na jimbo hilo la Koweït ambalo kwa kweli lilikuwa hapo zamani likimilikiwa na Baghdad.

Na huko Ulaya, nchi za upande wa mashariki Urusi, Yugoslavia, Tschekoslovakia na zinginezo kaingia miguu miwili katika siasa ya kidemokrasia zimoja kafikia kujigawa na kuunda nchi kazaa kulingana na ubaguzi wa lugha na kabila. Vita vikali, njaa, magonjwa na mengineo magumu yawaangamiza.

Tuwazavyo sisi, upendo na masikilizano tu ndio yatamaliza mizozo hiyo ambayo, ulimwenguni, watu wasiopenda amani wajaribu kuletea dunia yetu misukosuko ya kila aina na yasiyo na maana.

Mambo hayo yote yalitolewa kwenu na gazeti lenu tukufu "JUA" ingawa watu wengine walipendezwa kututusi, kutupinga na kututisha kwa njia mbalimbali. Gazeti lenu litaendelea kutuma mwangaza wa JUA popote mulipo. Kuhusu mwaka huu mpya, kiongozi-mhariri, bwana Mutiri-wa-Bashara, waandishi na watumishi wetu wote twawatakia nyinyi wasomaji wetu wapenzi, kila la heri, baraka na fanaka kwa mwaka huu mpya tulimo. MWAKA MPYA 1993.

André Bisimwa L-B. Tsereu